

# Safi na Salama?
## Maji na Usafi wa Mazingira

## 1. Utangulizi

Upatikanaji wa maji safi na salama ni mojawapo ya mahitaji ya msingi kwa binadamu wote. Swala hili linatiliwa mkazo katika malengo mahususi ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu. Lengo la sita la maendeleo endelevu linadhamiria kuona kuna upatikanaji wa maji safi na salama kwa wote ifikapo 2030.

Nchini Tanzania, jitihada za upatikanaji wa maji safi na salama zipo katika kila hatua ya MKUKUTA (Mkakati wa Kukukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania). Jitihada hizi pia zipo kwenye Dira ya Maendeleo Taifa (*Tanzania Development Vision 2025*), Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*) na katika ilani zote za uchaguzi za vyama vya siasa. Yapo makubaliano ya pamoja kwamba Maji ni kipaumbele cha muhimu lakini bado upatikanaji wa maji safi na salama hapa Tanzania umethibitika kuwa mgumu.

Tangu mwaka 2006, Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji *(The Water Sector Development Programme - WSDP)* unaogoza jitihada za serikali na wadau wa maendeleo kusambaza maji salama. Zaidi ya dola $1.2 bilioni zimetumika kati ya mwaka 2013 na mwaka 2016. Juhudi hii iliongezewa nguvu na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa ambayo iliuweka usambazaji wa maji katika vipaumbele sita vya awali.

Muhtasari huu unawasilisha takwimu juu ya upatikanaji wa maji, njia za kutibu maji na usafi wa mazingira kwa ujumla. Takwimu hizi zinajibu maswali kama je, jitihada na uwekezaji katika Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji na ule wa Matokeo Makubwa Sasa vimeleta tija katika kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama na usafi wa mazingira kwa wananchi? Je, ni njia kuu zipi za kutibu maji zinazotumiwa na wananchi? Je, ni wananchi wangapi walioshiriki kwenye kampeni ya jamii ya kufanya usafi iliyohamasishwa na Rais Magufuli?

Muhtasari huu umeandikwa na umeandaliwa na Twaweza East Africa.

S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
simu: +255 22 266 4301 |
bp: uwazi@twaweza.org | www.twaweza.org/sauti



Twaweza ni sisi

Takwimu za muhtasari huu zinatokana na utafiti wa Twaweza wenye jina la *Sauti za Wananchi. Sauti za Wananchi* ni utafiti wenye uwakilishi wa kitaifa unaotumia simu za mkononi. Uwakilishi huu ni wa Tanzania bara. Maelezo zaidi juu ya utafiti huu yanapatikana katika tovuti ya www.twaweza.org/sauti. Kwa muhtasari huu, takwimu zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,808 kutoka katika mzunguko wa 14 wa *Sauti za Wananchi* uliofanyika mwezi wa kumi, 2016.

Matokeo muhimu ni:

- Asilimia 54 ya kaya za Tanzania zinapata maji kutoka katika vyanzo vilivyoboreshwa
- Upatikanaji wa maji safi vijijini haujaongezeka kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita
- Uchotaji maji bado ni zoezi linalochukua muda na kimsingi limebakia kuwa jukumu la wanawake na watoto
- Asilimia 60 ya kaya za Tanzania hutibu maji, na njia kuu inayotumika ni kuyachemsha maji
- Umbali: changamoto kuu zinazowakabili wananchi hasa wa vijijini ni vyanzo vichache vya maji pamoja na maji hayo kuwa machafu.
- Gharama za juu na usambazaji usio wa uhakika ndio changamoto kubwa zinazowakabili wananchi wanaoishi katika maeneo ya mijini

# 2. Mambo nane muhimu kuhusu maji na usafi wa mazingira Tanzania


## Jambo la 1: Kaya tano kati ya kumi zinapata maji kutoka katika chanzo kilichoboreshwa

Asilimia 54 ya kaya za Tanzania zinatumia maji kutoka katika chanzo kilichoboreshwa1 kama chanzo chao kikuu cha maji ya kunywa.

Asilimia 74 ya kaya za mijini na asilimia 46 ya kaya za vijijini zinapata maji safi na salama. Upo uhusiano wa karibu kati ya utajiri wa kaya na upatikanaji wa maji. Asilimia 75 ya kaya tajiri zinapata maji ikilinganishwa na asilimia 41 ya kaya masikini.

1 Maana halisi imepatikana katika uanishaji wa Kitaifa na wa kimataifa wa aina za vyanzo vya maji; aidha vyanzo vilivyoboreshwa au ambavyo havijaboreshwa. Vyanzo vya maji vilivyoboreshwa humaanisha maji ya bomba, maji ya visima na chemichemi vinavyolindwa pamoja na maji ya mvua yanayovunwa; kama inavyotafsiriwa na shirika la kimataifa la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Watoto (UNICEF) – *kwa ufafanuzi zaidi tazama-https://www.wssinfo.org/definitions-methods/watsan-categories/*

**Kielelezo cha 1: Je chanzo kikuu cha maji ya kunywa kwa kaya yako ni kipi?**





**Chanzo cha taarifa**: *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 14, (Octoba 2016)


Tukiangalia takwimu hizi kwa undani zaidi, kaya moja kati ya nne (asilimia 26) inatumia kisima kisicho salama kama chanzo chake kikuu cha maji ya kunywa. Kaya moja kati ya tano (asilimia 20) zinatumia maji ya mto, mfereji au kisima.

Katika maeneo ya mjini, maji ya bomba ndio chanzo kikuu cha maji ya kunywa (ikiwa asilimia 61 ya wananchi wanapata maji kwa njia hii), na kaya tatu kati ya kumi (asilimia 31) wakiwa na bomba za maji ndani ya kaya. Kaya mbili kati ya kumi (asilimia 21) zinapata maji kutoka kwenye mabomba ya majirani na kaya moja kati ya kumi (asilimia 9) kutoka katika mabomba ya hadhara.

Katika maeneo yote ya mijini na vijijini, chini ya asilimia moja ya kaya huhifadhi maji ya mvua kama chanzo chao kikuu cha maji ya kunywa.

**Kielelezo 2: Chanzo kikuu cha maji ya kunywa katika kaya yako ni kipi?**






**Chanzo cha taarifa**: *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 14, (Octoba 2016)

## Jambo la 2: Upatikanaji wa maji safi na salama haujaongezeka ndani ya kipindi cha miaka kumi iliyopita

Ili kupata picha halisi ya mwenendo wa upatikanaji wa maji, hasa katika maeneo ya vijijini, tunalinganisha takwimu juu ya upatikanaji wa maji kutoka awamu kadhaa za utafiti wa Sauti za Wananchi na takwimu zilizokusanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kupitia tafiti zake za kaya, pamoja na takwimu zilizoripotiwa na Wizara ya Maji (MoW) na matokeo yaliyoripotiwa na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN).

Mwenendo wa takwimu zilizokusanywa na NBS pamoja *na Sauti za Wananchi* zinanonesha kwamba upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya vijijini haujabadilika tangu mwaka 2015. Kati ya tafiti kumi na nne, kumi na mbili kati ya hizo zilikadiria kwamba kati ya asilimia 41 na asilimia 48 ya kaya zinatumia vyanzo vilivyoboreshwa kwa ajili ya maji ya kunywa.[2]


Hata hivyo, takwimu za *Sauti za Wananchi* zinanonesha kuwa upatikanaji wa maji umepungua kutoka asilimia 55 mwaka 2014 hadi asilimia 46 mwaka 2016.

Wizara ya Maji imeripoti kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa maji kati ya asilimia 50 na asilimia 60, na takwimu za Matokeo Makubwa Sasa pia zinaripoti ongezeko la kasi kutoka asilimia 40 mwaka 2013 hadi asilimia 67 mwaka 2015.[3]

2 *NBS takwimu za utafiti kutoka Mpango wa Pamoja ufuatiliaji utafiti (https://www.wssinfo.org/documents/) ni pamoja na Idadi ya Watu na Utafiti wa Afya (2005, 2010, 2016), Household Budget Survey (2007, 2012), Utafiti wa Viashiria vya VVU / UKIMWI na Malaria (2008, 2012), Living Standards Measurement Survey (2009, 2011), na sensa (2012);*

3 Takwimu kutoka Wizara ya Maji Open Data portal (http://bit.ly/2ju8a2e );BRN 2013, 2015 takwimu kutoka Open Data portal (2013 na 2015: http://bit.ly/2jbjjDZ ); BRN 2014 takwimu kutoka Wizara ya Maji (http://bit.ly/2jZQmiS)

**Kielelezo 3: Upatikanaji wa maji safi Tanzania vijijini tangu 2015**





**Chanzo cha taarifa**: *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 14, (Octoba 2016), *NBS, takwimu toka Mpango wa Pamoja wa ufuatiliaji (https://www.wssinfo.org/documents/) Idadi ya Watu na Utafiti wa Afya (2005, 2010, 2016), Household Budget Survey (2007, 2012), Utafiti wa Viashiria vya VVU / UKIMWI na Malaria (2008, 2012), Utafiti wa viwango vya maisha yaani Living Standards Measurement Study (2009, 2011), na sensa (2012); takwimu za Wizara ya Maji kutoka Open Data portal (http://bit.ly/2ju8a2e); BRN 2013, 2015 Data portal (2013 na 2015: http://bit.ly/2jbjjDZ); BRN 2014 takwimu kutoka Wizara ya Maji (http://bit.ly/2jZQmiS)*

## Jambo la 3: Kaya nne kati ya kumi katika maeneo ya vijijini Tanzania hutumia saa moja au zaidi kutafuta maji

Asilimia 43 wanapata maji ndani ya dakika thelathini zilizopendekezwa katika malengo ya kitaifa ikiwemo MKUKUTA. Asilimia 19 wanatumia kati ya dakika thelathini na sitini na asilimia 38 wanahitaji zaidi ya saa zima kupata maji.

Kwa maeneo ya mjini, asilimia 18 hutumia zaidi ya saa moja kutafuta maji na asilimia 10 huchukua kati ya dakika thelathini na saa moja. Hata hivyo, kaya nyingi katika maeneo ya mjini hutumia dakika thelathini kupata maji.

**Kielelezo cha 4: Inakuchukua muda gani kufika kwenye chanzo cha maji, kuchota maji na kurudi nyumbani?**





**Chanzo cha taarifa**: *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 14, (Octoba 2016)

## Jambo la 4: Kazi ya kuchota maji hufanywa na wanawake na watoto katika asilima 80 ya kaya

Mwanamke mkuu wa kaya au mke wa mkuu wa kaya ndiye anayewajibika kuchota maji kwenya asilimia 61 ya kaya. Zaidi ya hapo, katika kaya zingine (asilimia 16), wajibu huu hubebwa na watoto. Hakuna tofauti kubwa kati ya maeneo ya mjini na vijijini.

**Kielelezo cha 5: Je ni nani katika kaya yako mwenye jukumu la kuchota maji**




**Chanzo cha taarifa**: *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 14, (Octoba 2016)

Ifahamike kwamba takwimu hizi zinatokana na maoni ya wanakaya juu ya nani mwenye wajibu huo. Maoni haya hayakuthibitishwa. Inaweza kuwa sehemu kubwa ya kazi ya uchotaji maji ni ya watoto au wafanyakazi kwa kupewa agizo na mwanamke mkuu wa kaya.


## Jambo la 5: Umbali na uchache wa vyanzo vya maji ndio changamoto kuu katika upatikanaji wa maji vijijini

Asilimia 39 ya wananchi vijijini wanasema kwamba umbali wa vyanzo vya maji na asilimia 35 wanasema uchache wa vyanzo vya maji ni changamoto kuu zinazowakabili. Changamoto za ziada ni pamoja na uchafu wa maji (asilimia 32) na usambazaji wa maji usio wa uhakika (asilimia 28).

Katika maeneo ya mjini, usambazaji usio wa uhakika ni tatizo lililozoeleka na wengi, ambapo watu wanne kati ya kumi (asilimia 37), walilitaja tatizo hili. Gharama kubwa za upatikanaji wa maji pia ilitajwa na wengi (asilimia 27) pamoja na uhaba wa vyanzo vya maji (asilimia 26).

Usambazaji usio wa uhakika na uhaba wa vyanzo vya maji ni kati ya matatizo makubwa katika maeneo yote ya mjni na vijijini.

**Kielelezo cha 6: Zipi ni changamoto kuu mbili ambazo jamii yako inakabiliana nazo katika upatikanaji wa maji safi ya kunywa?**





**Chanzo cha taarifa**: *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 14, (Octoba 2016)

## Jambo la 6: Kaya sita kati ya kumi zimeripoti kutibu maji yao kabla ya kuyanywa

Asilimia 61 ya kaya za Tanzana zimeripoti kwamba wao hutibu maji yao ili yawe salama kwa kunywa. Nusu yao (asilimia 49) wameripoti kuyachemsha maji yao na robo (asilimia 27) wameripoti kuyachuja kwa kutumia kitambaa au ungo. Kaya moja kati ya kumi wameripoti kutumia kemikali kama *Waterguard* (asilimia 7) au chujio (asilimia 2).

Kuchemsha maji ni njia inayotumika zaidi katika maeneo ya mjini (asilimia 58 ya kaya) kuliko vijijini (asilimia 45). Hali hiyo pia imejitokeza kwenye matumizi ya kemikali ambayo ni asilimia 14 ya kaya za mjini wanaofanya hivyo ikilinganishwa na asilimia 5 ya kaya za vijijini.

**Kielelezo cha 7: Unatumia njia yoyote ili kuyafanya maji yako yawe salama kwa kunywa *(asilimia ya wananchi waliotaja njia zifuatazo)*[4]**




**Chanzo cha taarifa**: *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 14, (Octoba 2016)


## Jambo la 7: Wananchi saba kati ya kumi wameripoti kuwa mbunge wao aliwaahidi kwamba atawaletea miradi ya maji kipindi cha uchaguzi uliopita

Wananchi wengi (asilimia 69) wameripoti kuahidiwa miradi ya maji katika kipindi cha uchaguzi wa mwaka 2015


Robo tatu ya hao wanaoripoti kuahidiwa miradi ya maji wamesema ahadi hizo hazijatekelezwa. Lakini mtu asilimia 25 ya wahojiwa wameripoti kwamba wabunge wao walitekeleza angalau baadhi ya ahadi zao kwenye suala la miradi ya maji.

**Kielelezo cha 8: Ahadi za kampeni na utekelezaji wake**

**A**: ***Je, katika uchaguzi uliopita mbunge wako aliahidi miradi ya maji?***




**B**: ***Je, mbunge wako ametekeleza miradi ya maji kama alivyoahidi?***





**Chanzo cha taarifa**: *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 14, (Octoba 2016)

4 Miongozo na viwango vya kutibu maji kutoka Taasisi ya Afya Duniani (kiingereza): http://www.who.int/water_sanitation_health/hygiene/om/linkingchap6.pdf

## Jambo la 8: Wananchi nane kati ya kumi wameripoti kunawa mikono baada ya kutoka chooni

Wananchi nane kati ya kumi (asilimia 81) wameripoti kunawa mikono yao baada ya kutumia choo. Mtu mmoja kati ya watatu (asilimia 36) ameripoti kunawa mikono kabla ya kula, na watatu kati ya kumi (asilimia 28) walinawa mikono walipohisi kwamba mikono yao ni michafu.

**Kielelezo cha 9: Je ni katika mazingira gani ulipotumia sabuni kuosha mikono yako tangu wakati kama huu jana?**





**Chanzo cha taarifa**: *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 14, (Octoba 2016)

## Jambo la 9: Wananchi tisa kati ya kumi walishiriki katika zoezi la kufanya usafi tarehe tisa Desemba 2015

Zaidi ya wananchi tisa kati ya kumi (asilimia 93) waliripoti kwamba jamii yao ilifanya usafi tarehe 9 mwezi desemba 2015.

Wananchi tisa kati ya kumi (asilimia 87) wanaoishi mjini waliripoti kwamba zoezi la kufanya usafi wa mazingira kila mwezi linaendelea. Vijijini, ni wananchi sita kati ya kumi (asilimia 64) walioripoti kwamba zoezi hili bado linaendelea.

Kilelezo cha 10: Ushiriki wa jamii katika mazoezi ya usafi




**Chanzo cha taarifa**: *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 14, (Octoba 2016)

## 3. Hitimisho

Tangu mwaka 2007, serikali na wadau wa maendeleo wametumia zaidi ya $2.0 bilioni katika awamu ya kwanza na ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji (WSDP). Mpango huu ulitia mkazo katika usambazaji wa maji vijijini hasa kupitia Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ambao ulidai kuleta mafanikio ya kuridhisha.

Muhtasari huu unaibua maswali kadhaa juu la rasilimali zilizowekezwa na kama zimeleta faida zilizotarajiwa, na pia kama kweli BRN imetekeleza kama ilivyoripoti. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya vijijini Tanzania haujabadilika katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Hili ni jambo la kufikirisha.

Je, kuna uwezekano kwamba kiasi kikubwa cha pesa kimewekezwa katika sekta ya maji bila kuwa na tija? Au je, utafiti ujao wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) utaibua matokeo tofauti kabisa na haya?

Pamoja na tatizo la kupata maji salama kwa kiwango stahiki, muhtasari huu umebainisha changamoto nyingine zinazowakabili wananchi. Maji yako mbali sana vijijini – asilimia 57 za wananchi hutembea kwa muda usiopungua dakika 30 kuyapata maji. Na katika kaya nane kati ya kumi, maji kimsingi ni suala la kijinsia, ambapo mzigo wa kutafuta maji huwaangukia wanawake na watoto.

Wananchi wameliweka tatizo la maji katika vipaumbele vikuu vya kero ambavyo vinapaswa kutatuliwa na serikali. Wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015, wagombea walitambua umuhimu

wa kutatua tatizo hili sugu linalowakabili wapiga kura.
Hata hivyo, suala hili hujitokeza mara chache sana kwenye vyombo vya habari vya taifa. Na hata kama fedha nyingi zitatumika katika miradi inayoleta mabadiliko ya muda mfupi na kuwaridhisha wabunge na wananchi wao kwa kipindi hicho (na pia kutoa mianya ya rushwa) ni miradi ya muda mrefu itakayoonesha kama upatikanaji wa kweli utafikiwa.

Kufanya miradi iendelee kudumu ni jukumu zito na gharama yake imegawanywa kati ya jamii, serikali za mtaa, na Wizara ya maji. Hata hivyo, kuwahamasisha watu kutibu maji na kunawa mikono ni changamoto ya kielimu na sio hata suala la kifedha au la kihandisi. Linatuhusu sote.

Yapo matokeo chanya katika utafiti huu. Uamuzi wa Rais Magufuli kuanzisha utaratibu wa kitaifa wa kusafisha mazingira kila jumamosi ya mwisho wa mwezi unaendelea kuwahamasisha wananchi. (Utaratibu huo ulianza mnamo tarehe 9 Disemba 2015 badala ya sherehe za uhuru wa Tanzania) Wananchi wengi wanaendelea kutekeleza zoezi hilo. Moyo huu ukiendelea kuwepo kwa muda mrefu, utaleta matokeo chanya zaidi.